kia kuchoka sana

sababu za kufanya hivyo.

MAJIRA UK 3.



gellah

# Wavuvi waomba kuelimishwa sheria ya uvuvi

**Na Judith Ferdinand, Mwanza**

WAVUVI wa Mwalo wa Bwiru Kijiweni, Mtaa wa Bwiru Ziwani, Kata ya Pasiansi wilayani Ilemela mkoani Mwanza wameomba serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuwaelimisha mara kwa mara kuhusu Sheria ya Uvuvi Namba 22 ya Mwaka 2003.

Sambamba na kupeleka nakala ambazo zimeandikwa kwa lugha ya Kiswahili kwa kila Mwalo ili waweze kuifahamu na kuielewa.

Wakizungumza na Majira lilipotembelea mwaloni hapo baadhi ya wavuvi hao walisema, jambo hilo litawasaidia pindi maofisa husika wanapokuja kuwakamata au kufanya doria inakuwa rahisi wanarejea kwenye sheria watakazokuwa nazo.

Mmoja wa wavuvi katika mwalo huo, Esther Selemani alisema, changamoto walionayo ni wengi wao kutofahamu wala kuelewa sheria hiyo ya uvuvi inayosimamia sekta hiyo kuwa inazungumza nini hivyo kujikuta wakifanya shughuli zao kwa mazoe bila kujua wapi wanakosea na wapi wapo sahihi.

INAENDELEA UK. 7

Scanned with CamScanner

ugonjwa wa

za simu ikiwa ni 0783 480 463 na 068 276 1164," alisema Mlwale.

MAJIRA UK 10



...i vya kujikinga na ...alikabidhiwa Dkt.

# ...gozi bora

...azazi kuwa na ...kuwashirikisha ...ngazi za maamuzi ...kujenga viongozi ...wa siku za baadaye. ...utaratibu wa ...watoto katika ...wakiwa viongozi ...kufanya maamuzi ...ha wengine, jambo ...wa na viongozi ...wawajibikaji kwa wale ...goza," alisema.

# Jamii yahimizwa kunywa maziwa ya mifugo

**Na Mwandishi Wetu, Siha**

MKURUGENZI wa Kituo cha Utafiti wa Mifugo kilichopo Westi Kilimanjaro, wilayani hapa, Nguluma Athumani ameitaka jamii kuwa na mazoea ya kutumia maziwa, yatokanayo na mifugo kwa kuwa ni kinga katika miili dhidi ya magonjwa.

Akizungumza katika shamba la Dahir Yussuf, katika Kata ya Kia wilayani hapa ambaye ni mfugaji wa ngamia alisema, maziwa ya ngamia yana virutubisho vingi kuliko maziwa ya dukani.

"Maziwa ni mlo kamili kwa kuwa yamebeba virutubisho vya aina zote vinavyohitajika katika mwili wa binadamu, kwani mtu anapokunywa maziwa kwa wingi yana faida ya kuujenga mwili pamoja na kinga ya magonjwa," alisema Athumani.

Kuhusu maziwa ya ngamia, alisema ni moja ya chakula muhimu chenye virutubisho vingi vyenye kinga ya magonjwa mbalimbali mwilini yakiwemo magonjwa ya UKIMWI, kisukari, vidonda vya tumbo, fizi kutoa damu na upungufu wa vitamini C,

Kwa upande wake Yussuf, alisema wanyama hao ni rafiki na wakulima kwani wakipita shambani hawali mazao kama walivyo wanyama wengine kama mbuzi na kondoo na kusababisha maafa.

"Ngamia ni rafiki wa mazingira kutokana na kwamba wanyama hao hawali mimea ya kupandwa, isipokuwa miti ya majani ya asilia kwani hawana kwato ambazo zingesababisha ardhi kuchimbika," alisema Yussuf.

Scanned with CamScanner

Mchuuzi wa biashara ndogo ambaye jina lake halikupatikana, akitafuta wateja wa barakoa na biashara ya mabegi katika Barabara ya Tabora jijini Dodoma jana. Uwapo wa ugonjwa wa Covid-19 unaosababishwa na virusi vya corona, umetoa fursa kwa kundi hilo la wajasiriamali kuchangamkia soko la barakoa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

elimu kwa waumini wao kwa vitendo ili kuwanusuru na maambukizo ya ugonjwa huo.

NIPASHE UK 15.

# *Mradi maalum wa utafiti malisho mifugo waanza*

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), Kituo cha Hombolo kwa kushirikiana na Shirika la Advanta Seed International, wameanza kutekeleza mradi maalum wa kutafiti na kuzalisha mbegu bora za malisho ya mifugo.

Akizungumza na Nipashe katika ziara maalum ya kutembelea mashamba ya utafiti wa mbegu hizo, Mzalishaji Mbegu Mkuu wa Kituo hicho, Dk. Lameck Nyaligwa, alisema mradi huo wa mwaka mmoja utafanya utafiti wa mbegu hizo kwenye mazao ya mtama na uwele.

Alisema mradi huo unatarajia kuleta mapinduzi makubwa katika sekta ya mifugo nchini.

Alizitaja aina za mbegu za mtama ambazo zipo katika mashamba hayo ya majaribio kuwa ni Sugar - Grace, Mega-Sweet, BMR Rocket na Jumbo-Gold.

"Mbegu hizi zinazalisha majani na miti yenye virutubisho muhimu sana kwa ajili ya malisho ya wanyama, hususan katika kuongeza uzito wa mnyama pamoja na uzalishaji wa maziwa," alisema.

Pamoja na hayo, alisema mradi huo utakapopitishwa na wataalamu, utaongeza fursa za kiuchumi miongoni wa wakulima, wafanyabiashara na wafugaji.

"Mradi huu utakapopitishwa, utatoa fursa kwa wakulima kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania kuja kununua mbegu husika na kwenda kuzalisha malisho haya ya kisasa na kuyauza kwa wafugaji, hali ambayo itawaongezea kipato," alisema.

Dk. Nyaligwa alisema kituo kitafungua milango kwa kampuni kubwa nchini kwenda kununua mbegu hizo kwa ajili ya kulima katika mashamba makubwa na baadaye kuyasindika majani hayo ili kuyauza katika maeneo mbalimbali ya ndani na nje ya nchi.

Diwani wa Hombolo Bwawani, Ased Ndajilo, alisema mradi huo unatarajiwa kuleta mapinduzi makubwa kwa wafugaji na wakulima nchini.

Aliwataka wafugaji na wakulima wote nchini kuchangamkia fursa hiyo muhimu, mara tu mradi huo utakapopitishwa na wataalamu husika.

Monica Malundo, mkazi wa kata hiyo, alisema mfumo wa mazao ya malisho utapunguza kasi ya ufugaji wa kuhamahama kwa ajili ya kutafuta malisho.

Alisema wafugaji wengi wamekuwa wakilisha mifugo yao kwa kutafuta malisho, hivyo kutokana na utafiti uliofanywa na TARI-Hombolo kubaini mazao bora ya malisho, utakuwa mkombozi mkubwa kwa wafugaji na watakuwa wanafuga kwa tija.